# UNEP@50

## Zana

Zana hizi zina kibali cha kutumika kuanzia Juni mwaka wa 2021 hadi Juni mwaka wa 2022 tu

# Jiunge nasi katika maadhimisho ya miaka 50 ya Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa

Wakati wa kikao cha tano cha Baraza la Umoja wa Mataifa kilichoendeshwa mtandaoni Februari 22-23, mwaka wa 2021, Nchi Wanachama ziliamua kuitisha kikao maalum cha kuadhimisha miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP). UNEP ilianzishwa mwaka wa 1972 kutokana na Kongamano la Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira ya Binadamu mjini Stockholm, lililofanya mazingira kuwa suala kuu la kimataifa kwa mara ya kwanza.

Tukio hili muhimu la kihistoria, linalojulikana kama UNEP@50, litaadhimishwa kuanzia tarehe 3 hadi 4 Machi mwaka wa 2022, punde tu baada ya kikao cha Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEA 5.2), kitakachofanyika kuanzia tarehe 28 Februari hadi tarehe 2 Machi.

Zaidi ya hayo, kuanzia tarehe 2 hadi tarehe 3 mwezi wa Juni mwaka wa 2022, mkutano wa kimataifa unaojulikana kama "Stockholm+50: sayari bora kwa ustawi wa wote – wajibu wetu, fursa yetu" (Stockholm+50) utaendeshwa mjini Stockholm, Uswidi, kama ilivyoamuliwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa katika kikao chake cha 75.  Baraza Kuu liliamua kuwa mkutano huu wa kimataifa unapaswa kuimarisha UNEP@50, kwa kuepuka maingiliano na kujirudiarudia.

Tunapoelekea UNEP@50, tunahimiza Nchi Wanachama kushiriki katika maadhimisho kwa kuonyesha masuluhisho, shughuli na mafanikio yao kuhusiana na masuala nyeti ya mazingira.

## Kwa nini ushiriki?

Kwa kipindi cha nusu karne iliyopita, UNEP imeratibu juhudi za kimataifa na Nchi zetu Wanachama ili kushughulikia changamoto kuu zaidi za mazingira duniani.

Tumeshirikiana kukarabati tabaka la ozoni, kukomesha matumizi ya mafuta yalio na risasi na kukomesha kuangamia kwa viumbe vilivyo hatarini kutoweka  haya ni baadhi tu ya mafanikio yetu. Uwezo wetu wa kuandaa mikutano umetoa jukwaa kwa nchi kujadiliana, kufanya uamuzi kwa ujasiri na kuendeleza ajenda ya mazingira duniani.

Nchi zetu Wanachama ni washirika muhimu katika utungaji wa sera ya UNEP, utekelezaji wa programu zetu na kupigania upatikanaji wa masuluhisho kwa changamoto zinazotukumba wote za mazingira.

Nchi Wanachama hutoa ufadhili wa kimsingi kwa UNEP kupitia kwa Mfuko wa Mazingira - nguzo ya kazi yetu ulimwenguni kote, tunaposaidia nchi kutekeleza vipengele vya mazingira vya Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu.

-
Kwa kuchangia pakubwa, nchi huheshimu ahadi zake za kushughulikia mazingira duniani kwa ushirikiano na mataifa mengine na asili.

UNEP@50 inatoa fursa ya kuimarisha tena ushirikiano wa kimataifa na kuchochea hatua za pamoja za kushughulikia changamoto tatu kwa sayari za mabadiliko ya tabianchia, uharibifu wa mazingira na bayoanuai, na uchafuzi na taka.

Hakuna nchi au bara linaloweza kutatua changamoto za kimataifa bila kusaidiwa. Lakini kila taifa lina wajibu muhimu wa kutunza watu na sayari yetu. Tunawahimiza kusimulia visa vyenu na kuwahimiza wengine kusaidia kubadilisha uhusiano wetu na mazingira.



## Maangazio ya UNEP@50

**UNEP@50 itaangazia jinsi ya kuimarisha zaidi msingi wa UNEP wa sayansi na uongozi kwa kuimarisha:**

- Kazi ya UNEP ya kukuza sera ya sayansi ya mazingira ili kuunga mkono na kutoa ushahidi wa hitaji la sera na mifumo dhabiti ya kimataifa, kulingana na mapendekezo ya Kamati ya Uendeshaji kuhusu mustakabali wa Hali ya Mazingira Duniani.
- Wajibu wa UNEP wa kuchochea utekelezaji wa makubaliano ya mazingira kama sehemu ya Ajenda ya 2030 kwa kukuza mfumo wa kusimamia mazingira unaoongozwa kupitia ubia wa washikadau mbalimbali ili kuwezesha ushirikiano wa kimataifa ambapo uwezo wa kuleta mabadiliko utashirikishwa katika sekta zote kwenye jamii.
- Wajibu wa UNEP kama nguzo ya kimataifa ya mazingira ndani ya mfumo wa Umoja wa Mataifa na kuimarisha hadhi ya Makao Makuu yake mjini Nairobi kama kitovu cha mazingira duniani.
- Uwezo wa kifedha wa UNEP kutimiza wajibu wake na kutekeleza Mkakati wake wa Mda ulioidhinishwa, wajibu wake na programu ya Kazi.

## Unaweza kufanya nini kuadhimisha UNEP@50?

**Shiriki katika UNEP@50 na uonyeshe jinsi Serikali yako imekuwa sehemu ya juhudi za kimataifa za kukuza utunzaji wa mazingira kwa kushiriki visa vya mafanikio yenu.**

**Unaweza kushiriki maadhimisho na kuweza kusikika kwa kuhamasisha kuhusu mazingira:**

**Tunapoelekea maadhimosho ya UNEP@50, unaweza:**

- Tumia hashtagi #UNEP50 kushiriki kwenye mazungumzo mtandaoni.
- Chapisha visa vya mafanikio kwenye tovuti yako na kwenye mitandao yako ya kijamii na kutumia Maafisa wa UNEP wa Mawasiliano ya Kanda (tazama Kiambatisho kufahamu jinsi ya kuwafikia).
- Fanya kazi na Maafisa wa UNEP wa Mawasiliano ya Kanda kutoka eneo lako kuchapisha makala muhimu, maoni au kufanya mahojiano na wataalamu katika vyombo vya habari vya ndani ya nchi na vya kimataifa.
- Shiriki visa kwenye tovuti yako na kwenye mitandao ya kijamii kuhusu jinsi ambavyo nchi yako imeshirikiana na UNEP na/au umuhimu wa UNEP kwa nchi yako katika kipindi cha miaka 50 iliyopita.
- Toa makala ya kweli, tafiti na rasilimali nyinginezo kuhusu masuala muhimu ya mazingira katika jamii, jiji, eneo au nchi yako. Tazama rasilimali za UNEP kupata sayansi na data ya hivi karibuni.
- Buni na ushiriki kadi katika mitandao ya kijamii zinazoangazia nukuu kutoka kwa watu mashuhuri wa eneo unalotoka au wa kitaifa, wataalam au Mawaziri kuhusu umuhimu wa kukabiliana na changamoto za aina tatu duniani. Pakua vielelezo vya UNEP@50 hapa.

**Wakati wa maadhimisho ya UNEP@50 kuanzia tarehe 3 hadi 4 Machi mwaka wa 2022, unaweza:**

- Fuata maadhimisho hayo mtandaoni. Maelezo zaidi yatatolewa tarehe ikiwa karibu kufika.
- Fuata akaunti za UNEP kwenye mitandao ya kijamii na kwenye YouTube ili upate masasisho ya moja kwa moja kuhusu UNEP@50 na ushiriki habari hizo kwenye akaunti zako za kidijitali.
- Toa ahadi ya ufadhili au kubuni kwa sera mpya ya mazingira katika jiji lako, eneo au nchi yako.



## Kile kitakachofanywa na UNEP ili kueneza ujumbe

- UNEP itaangazia visa vyenu, hati za kushuhudia kazi njema na ujumbe kwenye majukwaa yetu ya kidijitali.
- Kuanzia Oktoba mwaka wa 2021, utaweza kufikia rasilimali kwenye mitandao ya kijamii, zana za kidijitali na kadhalika kukusaidia kueneza habari kuhusu UNEP@50 tunapoelekea hafla kuanzia tarehe 3 hadi 4 Machi mwaka wa 2022 na kuendelea. Tembelea Trello hapa.
- UNEP imefanya utafiti kuhusu hatua muhimu za mazingira katika kipindi cha miaka 50 iliyopita na inaandaa mfululizo wa hadithi zinazochapishwa mara mbili kwa wiki kwenye tovuti ya UNEP. Inajumisha video, makala yaliyoandikwa, interaktivu na maudhui mengine bunifu. Angalia ukurasa wa tovuti wa UNEP@50 mara kwa mara na ushiriki hadithi hizo kwenye mifumo yako ya kidijitali.

## logo ya UNEP@50

- Nchi Wanachama zinahimizwa kuhamasisha kuhusu UNEP@50 kwa kutumia nembo rasmi.
- Nembo ya UNEP@50 kwenye lugha mbalimbali na maagizo ya jinsi ya kuitumia yanaweza kupatikana hapa.

## Kiambatisho: Ujumbe Mkuu wa UNEP@50

**Kwa ujumla**

- Mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira na bayoanuai, na uchafuzi na taka vinajumuisha masuala matatu yanayochangia changamoto tatu duniani zinazoingiliana ambazo ni tishio lisilokubalika kwa kizazi kilichopo na kijacho.
- Juhudi kabambe zilizoratibiwa kutoka kwa serikali, mashirika ya biashara na watu kote duniani zinaweza kuzuia na kubadili athari mbaya zaidi za kuzorota kwa mazingira kwa kubadilisha mifumo muhimu kwa haraka, ikijumuisha nishati, maji na chakula, ili matumizi yetu ya ardhi na bahari yawe endelevu.
- Kubadilisha mifumo ya kijamii na kiuchumi ni sawa na kuboresha uhusiano wetu na mazingira, kuelewa thamani yake na kuzingatia thamani yake kama msingi wa kufanya maamuzi yetu.
- Sayansi ni muhimu ili kushughulikia baadhi ya masuala nyeti ya uendelevu katika karne ya 21 na kuhakikisha ufanyaji maamuzi na sera zinategemea ushahidi.

**Wajibu wa UNEP**

- Kwa kipindi cha miaka 50, UNEP imekuwa mstari mbele kutunza mazingira kupitia kuelimisha, kuwezesha na kuchochea mataifa na watu kuimarisha maisha yao bila kuhatarisha yale ya vizazi vijavyo.
- UNEP hutoa masuluhisho na maelekezi ya kisayansi kuhusu sera nzuri na sheria mwafaka za mazingira ili kuimarisha afya ya binadamu na kuboresha sayari.
- UNEP hujengea Nchi Wanachama uwezo ili kuwa na matokeo endelevu kwenye sera ya sayansi, sheria na usimamizi na uvumbuzi wa kiteknolojia.
- Kama msimamizi mkuu wa masuala ya mazingira duniani, UNEP ndiye mhusika pekee wa kimataifa aliye na wajibu na uwezo wa kuleta pamoja mataifa, viongozi wakuu, mashirika ya biashara na mashirika ya uraia ili kukabiliana na changamoto kuu za mazingira tunazoshuhudia kwa sasa.
- Kupitia kampeni zake, UNEP huhamasisha na kupigania hatua mwafaka kuhusiana na changamoto kuu za mazingira.
- Ndani ya jamii ya Umoja wa Mataifa, UNEP hushughulikia kipengee cha mazingira cha maendeleo endelevu. UNEP itatumia fursa ya Mageuzi ya Mfumo wa Maendeleo ya Umoja wa Mataifa kupanua ufikiaji wake kama mhamasishaji mkuu wa masuala ya mazingira duniani ili kusaidia Nchi Wanachama zinapojitahidi kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu.



**Maendeleo yasiyo endelevu yanapunguza kwa kasi uwezo wa Dunia kumudu mahitaji ya binadamu**

Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita, uchumi duniani umekua angalau mara tano, kutokana na kuongezeka mara tatu kwa uchimbaji wa maliaghafi na nishati ambavyo vimeongeza uzalishaji na matumizi ya bidhaa.

**Dunia inashindwa kutimiza ahadi zake za kupunguza uharibifu wa mazingira**

- Dunia inaelekea kushuhudia ongezeko la joto la angalau nyuzijoto 3, kiwango cha juu kuliko viwango vya kabla ya viwanda kufikia 2100. Hii inamaanisha kukosa kufikia lengo la Mkataba wa Paris wa kufanya ongezeko la joto lisizidi nyuzijoto 2 na kujaribu kudhibiti ongezeko hilo lisizidi 1.5 ili kuepuka athari mbaya zaidi.
- Hatua za pamoja kwa dharura zinahitajika ili kukabiliana na changamoto za aina tatu zinazoikabili dunia za mabadiliko ya tabianchia, uharibifu wa mazingira na bayoanuai, na uchafuzi na taka.

**Kudorora kwa mazingira kunapunguza kasi ya kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu**

- Mabadiliko ya kimazingira ni kizingiti kwa kutokomeza umaskini na baa la njaa, kutoa maji safi na usafi, kupunguza ukosefu wa usawa, kukuza uchumi kwa njia endelevu, na kukuza jamii zilizo na amani na umoja.
- Haki ya kuwa na mazingira salama, safi, bora na endelevu inatambuliwa kisheria katika nchi 155. Mazingira bora ni muhimu ili kufurahia kikamilifu haki mbalimbali za binadamu, ikiwa ni pamoja na haki za afya, chakula, maji, na usafi.

**Changamoto za mazingira zinazoingiliana Duniani zinapaswa kushughulikiwa kwa pamoja**

- Maingiliano kati ya mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa bayoanuai, uharibifu wa ardhi, na uchafuzi wa hewa na maji ni ishara kuwa vinapaswa kushughulikiwa kwa pamoja ili kuongeza manufaa na kupunguza gharama.

**Maarifa ya binadamu, werevu, teknolojia na ushirikiano vinaweza kubadilisha jamii na uchumi na kuwezesha kuwa na mustakabali endelevu**

- Mabadiliko ya mfumo mzima yanaweza kuwezesha ustawi kwa wote kuzingatia uwezo wa Dunia wa kukidhi maisha, kutoa rasilimali na kufyonya taka. Mabadiliko yanahusisha mabadiliko ya kimsingi kwenye teknolojia, uchumi na mfumo wa jamii, ikijumuisha mitazamo ulimwenguni, kanuni, maadili na usimamizi.

**Mifumo ya kiuchumi na kifedha iliyofanyiwa mabadiliko inaweza kuongoza mabadiliko endelevu**

- Serikali zinapaswa kujumuisha uwajibikiaji kikamilifu wa malighafi wakati wa kufanya maamuzi na kutoa motisha kwa mashirika ya biashara kufuata mkondo. Mambo msingi kama vile mali jumla ni muhimu kuliko pato la taifa wakati wa kupima maendeleo endelevu ya kiuchumi.
- Serikali zinapaswa kujumuisha mtaji wa malighafi katika hatua za utendaji wa kiuchumi. Zinapaswa kuweka bei ya kaboni, kuondoa ruzuku hatari, na kuelekeza upya sehemu ya zaidi ya dola za Marekani trilioni 5 za ruzuku za kila mwaka kwa fueli ya visukuku; kilimo na uvuvi usio endelevu; nishati isiyojadidifu; uchimbaji madini, na uchukuzi ili kupunguza gesi ya ukaa na kutoa masuluhisho yanayojali mazingira.

**Kila mtu ana wajibu wa kutekeleza kuleta mabadiliko yatakayowesha mustakabali endelevu**

- Wahusika wote wana wajibu kama watu binafsi, unaoingiliana na kuwiana, wa kutekeleza ili kuleta mabadiliko kwenye sekta mbalimbali na kwenye uchumi yalio na athari za mda na za kudumu.
- Watu binafsi wanaweza kuleta mabadiliko kwa kujifunza kuhusu uendelevu, kupiga kura na kutekeleza haki yao ya kiraia, kubadilisha milo yao na njia za usafiri, kutoharibu chakula na rasilimali, na kupunguza matumizi yao ya maji na nishati.
- Kupitia ushirikiano wa kimataifa, sera na sheria, serikali zinaweza kuwa mstari mbele kusababisha mabadiliko kwa jamii na kwa uchumi wetu.
- Sekta ya kibinafsi, taasisi za fedha, mashirika ya ajira, mashirika ya kisayansi na elimu, vyombo vya habari, familia na mashirika ya kiraia yanaweza kuanzisha na kuongoza mabadiliko katika nyanja zao.



## Kiambatisho: Tovuti zilizo na rasilimali/zana muhimu

**Tovuti ya kuwepo kwa UNEP@50:** www.unep.org/unep-50

**Ratiba ya matukio ya UNEP@50:** www.unep.org/who-we-are/about-us/environmental-moments-unep50-timeline

**Video ya maadhimisho ya UNEP@50:** https://www.youtube.com/watch?v=GDfXFv6JIU8

**Trello bodi na makala ya kidijitali ya UNEP@50:** https://trello.com/b/b6iULwv7/unep-50

**Tovuti ya Stockholm+50:** https://www.stockholm50.global/

## Kwa mawasiliano

**Maafisa wa Umoja wa Mataifa wa Mawasiliano ya Kanda:**


**Asia na Pasifiki**
Mayan Mojado / mojado@un.org

**Afrika**
Mohamed Atani / mohamed.atani@un.org

**Ulaya**
Alejandro Laguna / laguna@un.org

**Amerika ya Latini na Karibiani**
Elisa Vásquez / elisa.vasquez@un.org

**Amerika Kaskazini**
Laura Fuller / laura.fuller@un.org

**Asia Magharibi**
Noora Albinkhalil / noora.albinkhalil@un.org

**Mkurugenzi wa Mawasiliano wa UNEP**
Daniel Cooney / unep-communication-director@un.org

**Ofisi ya Masuala ya Usimamizi wa UNEP**
Ulf Björnholm Kaimu Mkurugenzi / ulf.bjornholm@un.org

**Ofisi ya Utendaji wa UNEP**
Juan Bello Afisa Mratibu Mwandamizi / juan.bello@un.org







**Tafadhali kumbuka matumizi ya zana hizi yanaambatana na kanusho lifuatalo.**

Kanusho: Matumizi ya nembo ya UNEP@50 haimaanishi uidhinishaji wa mtumizi, bidhaa zao, huduma au shughuli zake, au maudhui ya tovuti yake au tovuti zilizounganishwa au usahihi wa taarifa, maoni au kauli zinazotolewa.